

Mahojiano ya CRAFFT 2.1

Kupewa kwa mdomo na tabibu

Anza: “Nitakuuliza maswali machache ambayo ninawauliza wagonjwa wote. Tafadhali sema ukweli. Nitayaweka siri majibu yako.”

Sehemu ya A

Kipindi cha MIEZI 12 ILIYOPITA, ni kwa siku ngapi:

- | | |
|--|----------------------|
| 1. Ulikunywa mafunda zaidi ya bia, mvinyo, au kinywaji chochote kilicho na pombe? Sema “0” ikiwa hamna. | <input type="text"/> |
| | Siku # |
| 2. Ulitumia marijuana (bangi, mafuta au nta kwa kuvuta, kufusha, kutona au katika vyakula) au “ marijuana ya kusanisi ” (kama “K2,” “Spice”)? Sema “0” ikiwa hamna. | <input type="text"/> |
| | Siku # |
| 3. Ulitumia kingine chochote kulewa (kama vile dawa haramu, dawa za maagizo na zisizo za maagizo na vitu unavyonusa, kupumua, kufusha, au kujidunga)? Sema “0” ikiwa hamna. | <input type="text"/> |
| | Siku # |

Je, mgonjwa alijibu “0” kwa maswali yote katika Sehemu ya A?

Ndiyo



Uliza swali la GARI pekee, kisha uache

Hapana



Uliza maswali yote 6 ya CRAFFT katika Sehemu ya B

Sehemu ya B

Chorea mduara moja

- | | | |
|---|--------|-------|
| C Umewahi kupanda GARI linaloendeshwa na mtu (ikiwemo wewe mwenyewe) aliyekuwa “mlevi” au alikuwa akinywa pombe au kutumia dawa za kulevya? | Hapana | Ndiyo |
| R Je, unakunywa pombe au unatumia dawa za kulevya KUTULIA , kuhisi vizuri kujihusu, au kufaa? | Hapana | Ndiyo |
| A Je, unakunywa pombe au unatumia dawa za kulevya ukiwa PEKE YAKO ? | Hapana | Ndiyo |
| F Je, UNASAHU mambo uliyofanya unapokunywa pombe au kutumia dawa za kulevya? | Hapana | Ndiyo |
| F Je, FAMILIA au MARAFIKI zako hukuambia kuwa unapaswa kupunguza kulewa au kutumia dawa za kulevya? | Hapana | Ndiyo |
| T Je, umewahi kujipata MATATANI ukinywa pombe au ukitumia dawa za kulevya? | Hapana | Ndiyo |

Majibu mawili au zaidi ya NDIYO yanaashiria tatizo kubwa na haja ya tathmini zaidi.

Tazama Ukurasa wa 3 kwa maagizo zaidi.




NOTISI KWA WAFANYAKAZI WA KLINIKI NA REKODI ZA MATIBABU:

Taarifa zilizo kwenye ukurasa huu zimelindwa na kanuni maalum za usiri za serikali kuu (42 CFR Sehemu ya 2), ambazo zinapiga marufuku ufichuaji wa taarifa hizi isipokuwa iwe imeidhinishwa kwa kibali maalum cha maandishi.

Ukalimani wa Alama za CRAFFT

Uwezekano wa Maradhi ya Matumizi ya Mihadarati ya DSM-5 na alama za CRAFFT*



Chanzo cha data: Mitchell SG, Kelly SM, Gryczynski J, Myers CP, O'Grady KE, Kirk AS, na Schwartz RP. (2014). Alama za thamani za CRAFFT na vigezo vya DSM-5 vya pombe na dawa nyingine: tathmini na uchunguzi mwingine. Matumizi ya Dawa za Kulevya, 35(4), 376–80.

Tumia sehemu za 5 R za kuzungumzia kwa ushauri nasaha mfupi.



1. PITIA matokeo ya uchunguzi

Kwa kila jibu la “ndiyo”: “Unaweza kunipa maelezo zaidi kuhusu hilo?”



2. PENDEKEZA kutotumia

“Kama daktari wako (muuguzi/mhudumu wa afya), pendekezo langu ni kutokunywa pombe, kutotumia nikotini, marijuana au dawa nyingine za kulevya kwa sababu zinaweza: 1) Kudhuru ubongo wako unaokua; 2) Kuhitilafiana na masomo na kumbukumbu, na 3) Kukuabisha au kukuweka katika hali hatari.”



3. KUENDESHA GARI ushauri nasaha wa hatari

“Migongano ya magari ni chanzo kinachoongoza cha vifo vya vijana. Ninawapa wagonjwa wangu wote Kandarasi ya Maisha. Tafadhali ipeleke nyumbani na ujadili na wazazi/walezi wako ili kuunda mpango kwa ajili ya safari salama kuelekea nyumbani.”



4. JIBU shawishi kauli za kujimotisha

Wasio watumiaji: “Mtu akikuuliza kwa nini hunywa pombe, kufusha, au kutumia tumbaku au dawa za kulevya, utasema nini?” Watumiaji: “Je, kuna manufaa gani kwa kutotumia?”



5. MARISHA imani

“Ninaamini kuwa una uwezo wa kuzuia matumizi ya mihadarati kuwa kizingiti cha kutofanikisha malengo lengo.”

Mpe mgonjwa Kandarasi ya Maisha. Inapatikana kwenye www.crafft.org/contract

© John R. Knight, MD, Boston Children's Hospital, 2020.

Imezalishwa tena kwa ruhusa kutoka Center for Adolescent Behavioral Health Research (CABHRe), Boston Children's Hospital.

crafft@childrens.harvard.edu www.crafft.org

Kwa taarifa zaidi na matoleo katika lugha nyingine, tazama www.crafft.org.